Agosti 2018

United Nations TANZANIA Delivering as One



# Programu ya Pamoja ya Zanzibar


## MUHTASARI MKUU

Ushirikiano wa miaka iliyopita na wa sasa kati ya Ofisi ya Umoja wa Mataifa nchini na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar umedhihirisha kwamba Zanzibar ina fursa muhimu kwa maendeleo ya jamii na ukuaji wa kiuchumi, zikiwemo sekta za kilimo cha baharini na utalii. Hata hivyo, ni muhimu kukiri kwamba Zanzibar inakabiliana na changamoto kubwa za kimaendeleo. Hivi sasa, asilimia 30.4 ya watu wa Zanzibar wanaishi chini ya kizio cha umaskini wa mahitaji muhimu, ambapo asilimia 10.8 wanaishi chini ya kizio cha umaskini. Vilevile, kuna kasi kubwa sana ya ukuaji wa idadi ya watu ambapo ifikapo mwaka 2050, idadi inakadiriwa itakuwa mara mbili ya ile iliyopo sasa. Kiwango cha ukosefu wa ajira, hasa miongoni mwa vijana, kimeongezeka. Kwa kiasi fulani bado kuna haja ya kuimarisha mahitaji ya msingi, yakiwemo kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama, usafi na huduma za afya. Vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto bado si jambo geni Zanzibar ambapo data zinaonyesha kwamba kuna ongezeko la vitendo hivyo kimwili, kingono na kihisia.

Mashauriano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yamefanyika kuhusu mahitaji na vipaumbele vyake, pamoja na uchambuzi wa takwimu zilizopo, na pia mapitio juu ya namna UN inavyoweza kutoa mwitikio kwa mahitaji haya. Programu hii iliyojikita katika eneo maalumu ni matokeo ya mashauriano na inahusisha mashirika tisa ya Umoja wa Mataifa, yaani, FAO, ILO, IOM, UNDP, UNFPA, UNICEF, UNIDO, UN Women na WHO.

Programu hiyo inalenga katika maudhui (maeneo) manne makuu: Afya ya Mama na Mtoto Mchanga; Uwezeshaji Kiuchumi wa Wanawake kupitia Uendelezaji wa Mnyororo wa Thamani katika Kilimo cha Mwani; Kukomesha Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto; na Kujenga Uwezo kwa ajili ya Uratibu na Utoaji Taarifa juu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Mkakati wa Kupunguza Umaskini na Ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar (Mkuza III). Kuna uhusiano wa karibu kati ya matokeo yote yanayotegemewa katika programu hii na maudhui yote yamezingatia masuala ya jinsia. Uratibu wa SDGs na utoaji taarifa zake unaweka msisitizo katika maudhui yote kwa kuzingatia upana wa SDGs lakini pia haja ya kuimarisha takwimu na data.

## HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA




- IMEFADHILIWA: 6.5M
- HAIJAFADHILIWA: 27.5M
- JUMLA: 33.8M

### Imefadhiliwa na

- Canada
- Japan
- Sweden
- Norway
- Mifuko mingine kutoka makao makuu ya UN

## Mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayoshiriki

UNDP — Empowered lives. Resilient nations.
UNFPA
International Labour Organization
Food and Agriculture Organization of the United Nations
unicef — for every child
UNIDO
IOM — UN MIGRATION
World Health Organization
UN WOMEN — United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women



# Afya ya Mama na Watoto Wachanga

## Shirika Linaloongoza

UNFPA

**Batula Abdi**
Mtaalamu wa Afya ya Uzazi na Akina Mama
abdi@unfpa.org

## Hali ilivyokwa sasa

**236** Vifo kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwaka 2015 (Viwango vya Vifo vya Akina Mama) huko Zanzibar.

**62%** ya vifo vya watoto wachanga Zanzibar ni vifo vya baada ya kuzaliwa.

**45** Vifo kwa kila vizazi hai 1,000 kwa mwaka 2015 (Vifo vya Watoto Wachanga) huko Zanzibar.

## Mwitikio

Mkazo wa mwitikio utakuwa katika hospitali mbili za Zanzibar—Mnazi Mmoja huko Unguja na Hospitali ya Chake Chake huko Pemba na pia uimarishaji wa mfumo mzima wa afya ili kutoa huduma bora kwa wanawake na watoto. Hospitali zote hizi mbili zinatoa matunzo ya afya kwa jamii nzima katika visiwa hivyo. Programu hii itaendeleza juhudi za awali za UN katika hospitali hizi mbili.

Mfumo wa afya ulioimarishwa kupitia ujenzi wa uwezo wa mameneja wa hospitali na misaada ya kiufundi kwa menejimenti na uongozi wa hospitali. Shirika la Zanzibar la Chakula na Dawa itawezeshwa katika kuwa na mfumo mzuri wa huduma za maabara na ufuatiliaji ili kusimamia ubora na uzingatiwaji wa viwango vya kimataifa kwa dawa zinazoagizwa kutoka nje.

Uwezo uliomarishwa kutengeneza data kwa ajili ya uwekaji mipango kwa kuzingatia ushahidi na kutoa uamusi. Programu itasaidia hospitali hizo mbili kukusanya, kuweka taarifa pamoja, kuchambua na kutumia data katika utaratibu wa kuaminika na kwa wakati. Ufuatiliaji wa Taarifa za Vifo vya Akina Mama Kabla na baada ya Kujifungua na uchukuaji hatua utasaidiwa ili kuhakikisha kwamba kila kifo cha kabla na baada ya kujifungua akina mama kinaingizwa katika kumbukumbu na hatua inachukuliwa.

Ubora wa matunzo kwa akina mama na watoto wao wachanga utaimarishwa kupitia msaada wa ujenzi wa uwezo wa watoa huduma za afya. Njia za kiubunifu zitatumika kujenga uwezo kama vile kuimarisha usimamizi, kuanzisha programu za utoaji mafunzo kwa vitendo, tiba kwa teknolojia ya mawasiliano na matumizi ya majukwaa ya kujifunza kwa njia za kimtandao.

Programu ya Afya ya Jamii kwa Kujitolea itaimarishwa kupitia kusajili na kutoa mafunzo kwa wale wapya wanaojitolea na mafunzo ya kuboresha ujuzi kwa wale wanaojitolea wapatao 1,800 walio kazini tayari. Kimsingi, programu hii ni muhimu ili kuongeza ujuzi kuhusu masuala ya afya miongoni mwa wanajamii ili kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi.

## Mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayoshiriki

UNFPA

unicef for every child

World Health Organization



# Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kupitia Kilimo cha Mwani

## Hali ilivyokwa sasa

Miongoni mwa changamoto kubwa ambazo wanawake wajasiriamali wa Zanzibar wanakabiliana nazo ni uwezo wa kijasiriamali, uwezo katika kuongeza thamani, miundo-dhana ya kisheria na miiko ya kijamii na kiutamaduni.

**30.4%** ya watu wazima Tanzania wanakipato chini ya kizio cha chini cha umaskini USD 1.25.

**48** Mamilioni ya Watanzania watahitaji kuingia kwenye soko la ajira ifikapo mwaka 2050.

## Shirika Linaloongoza

Food and Agriculture Organization of the United Nations


**Natalie Kapinga**
Mtaalamu wa Ufuatiliaji na Tathimini
natalie.kapinga@fao.org


## Mwitikio

Maudhui haya ya mnyororo wa thamani katika maendeleo ya kilimo cha mwani yanalenga kusaidia kuleta mabadiliko ya uchumi, yakiwemo utoaji wa kazi zenye staha hasa kwa ajili ya uwezeshaji wanawake na vijana kiuchumi. Katika hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kusaidia Wizara, Idara na Wakala (MDAs) pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) zinazohusika na pia sekta binafsi ili kuendeleza uhamasishaji na uhusishwaji wa mnyororo wa thamani katika kilimo cha mwani. Mradi huo utawasaidia moja kwa moja jamii za wakulima wadogowadogo wa mwani, hasa vikundi vya wanawake na vijana wanaojishughulisha katika mnyororo huo mzima wa thamani. Malengo ni:

- Kuongeza tija na ujuzi wa kiujasiriamali kwa ajili ya uzalishaji endelevu wa mwani kama njia ya kujipatia kipato kwa wanawake na vijana.
- Kushajiisha mila za kijamii na kiutamaduni ambazo zinasaidia uwezeshaji wa wanawake na vijana kiuchumi.
- Kuimarisha ushirikishwaji wa sekta za umma na binafsi na katika uwekezaji kwenye kuongeza thamani kwenye kilimo cha mwani na masoko.
- Kuimarisha uwezo wa MDAs na LGAs ili kusaidia uwezeshaji wa wanawake na vijana kiuchumi katika mnyororo wa thamani wa kilimo cha mwani.

## Mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayoshiriki

Food and Agriculture Organization of the United Nations

International Labour Organization

UNIDO

UN WOMEN — United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women



# Kukomesha Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto

## Hali ilivyokwa sasa

**71%** ya wavulana na asilimia 62 ya wasichana wanasema wamewahi kufanyiwa ukatili wa kimwili kabla ya kutimiza miaka 18.

**35.5%** ya wanaume Zanzibar wanaamini kwamba kitendo cha kumpiga mwanamke ni halali kwa baadhi ya nyakati.

**18%** ya wasichana Zanzibar huwa wanaolewa kabla ya kutimiza umri wa miaka 18, na asilimia 3.5 kabla ya kutimiza miaka 15.

## Shirika Linaloongoza

unicef for every child


**Ahmed Rashid**
Mtaalamu wa Ulinzi kwa Watoto
aharali@unicef.org


## Mwitikio

Maudhui ya Kukomesha Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto yanawalenga wanawake na watoto wote wa Zanzibar (takribani watu 980,032). Programu itaendeleza maendeleo yaliyokwishafikiwa katika kukabili ukatili dhidi ya wanawake na watoto kupitia utekelezaji wa shughuli zilizochaguliwa na zinazohimizwa katika Mpango wa Taifa wa Kuchukua Hatua za Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Zanzibar (NPA-VAWC) (2017-2022). Mifano ya hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na:

- Kuhamasisha mabadiliko chanya katika mazingira ya kisheria na kibajeti ili kutoa kinga kwa wanawake na watoto kupitia mabadiliko ya kisheria, kujenga uwezo wa kitaasisi, na kuimarisha usimamizi wa data.
- Kuimarisha upatikanaji wa ubora wa huduma za kinga, kama vile matunzo ya dharura kwa watoto wenye mahitaji makubwa ya kinga, kushirikiana na maofisa wa mahakama ili kushughulikia kwa ufanisi mkubwa kesi zinazohusu vitendo vya ukatili na kujenga uwezo wa watoa huduma walio mstari wa mbele katika kubaini na kushughulikia kesi hizo.
- Programu ya kuzuia vitendo vya ukatili inayolenga kushughulikia vitendo vilivyo viovu kwa wanawake na watoto, ikiwemo kuanzisha mkakati madhubuti wa mawasiliano, kujenga uwezo wa wadau kushughulikia ndoa za utotoni na biashara haramu ya usafirishaji binadamu, kuunga mkono malezi bora katika familia, kutelekeza kwa vitendo dhana ya Shule Salama na kuanzisha mitandao ya mahalia ya kuunda vikundi vya wanawake vya masuala ya kiuchumi.

## Mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayoshiriki

unicef for every child | UNFPA | IOM UN MIGRATION | UN WOMEN United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women




# Uratibu na Utoaji Taarifa za Malengo ya Maendeleo Endelevu

## Shirika Linaloongoza

UNDP
Empowered lives. Resilient nations.

**Rukiya Wadoud**
Mtaalamu wa Menejimenti ya Programu na Operesheni
rukiya.wadoud@undp.org

## Hali ilivyokwa sasa

Jambo muhimu kwa ajili ya mafanikio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ni uwepo wa mifumo imara ya kitaifa, yenye uwezo unaojitosheleza, kuratibu utelekezaji na utoaji taarifa.

- Mashauriano na mapitio ya taarifa mbalimbali yameonyesha uwezo mdogo wa Zanzibar katika uratibu, usimamizi na utoaji taarifa kuhusu SDGs.
- Changamoto za uwezo kwa maana ya ubora, kutegemewa, muda na kufaa kwa data kutoka katika vyanzo mbalimbali vyote vimebainishwa.
- Seti nyingi za data hazina vipengele hivi muhimu: umri, jinsia, mahali na hadhi ya kijamii-kiuchumi.

## Mwitikio

Maudhui haya yataweka mkazo katika kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa Tume ya Mipango ya Zanzibar (ZPC) ambayo ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa SDGs na Mkuza III na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) ambayo ina dhamana ya masuala ya takwimu rasmi za Zanzibar. MDAs muhimu katika sekta, vyama vya kiraia (CSOs) vilivyoteuliwa na pia makundi ya wasomi yataimarishwa kwa kuzingatia nafasi zao katika kuzalisha data na kutekeleza na kusimamia SDGs na Mkuza III. Hatua muhimu za kuchukua ni pamoja na:

- Kuimarisha mfumo wa taifa wa uratibu ambao utaongoza utekelezaji, uratibu na utoaji taarifa za SDGs na MKUZA III huko Zanzibar.
- Kuanzishwa kwa kanzidata na muundo-dhana wa usimamizi unazingatia jinsia ili kuwezesha usimamizi wa viashiria vya SDGs, Haki za Watoto na MKUZA III.
- Kuanzisha na kuhamasisha mikakati ya kiubunifu ili kuhakikisha utayarishaji, usambazaji na matumizi sahihi ya data kwa ajili ya maendeleo endelevu. Hii ni pamoja na kuhamasisha mbinu za kuwasilisha data kwa ajili ya uchambuzi na usambazaji wa takwimu za SDGs.
- Kuanzisha miundo-dhana ya kiutawala na kitaasisi ambayo itawezesha mifumo ya takwimu ya Kitaifa kukidhi mahitaji na fursa za mifumo ya data inayotegemeana na inayobadilika.

## Mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayoshiriki

UNDP (Empowered lives. Resilient nations.) · UNFPA · unicef for every child · UN WOMEN (United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women)

United Nations

TANZANIA

Delivering as One

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi:

**Dorothy Temu-Usiri**

Mratibu wa Ofisi Ndogo za UN Zanzibar
Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa
P.O.Box 438
Mobile: +255 787 188 187
Email: dorothy.usiri@one.un.org